# CLASS 7 MID TERM 2 2020

# KISWAHILI

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU** **Muda: Saa 1 Dak. 40**

**(i) Tumia penseli ya kawaida**

**(ii) Hakikisha kuwa katika karatasi ya majibu umeandika:**

**(i) JINA LAKO** **(ii) JINA LA SHULE YAKO**

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1-15. Kwa kila nafasi chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliopewa**

Mganga __1__ ni methali __2__ tangu jadi. Hapo zamani za kale wanyama __3__ na simba. Wanyama __4__ sna mfalme __5__. Siku __6__ alipatwa na __7__ usiokuwa na __8__. Mfalme alipkuwa amelala, nyoka __9__ mdomoni akaenda __10__ tumboni __11__ nyoka alistarehe __12__. Hili __13__ Jambo la __14__ mno. Hata hivyo __15__ ya Musa utaona ya Firauni.

| | A. | B. | C | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | hajinyoi | hajikati | hajigangi | hajijui |
| 2. | za | ya | wa | la |
| 3. | walitawala | walitawalia | walitawala | walitawaliwa |
| 4 | waliwaogopa | walimuogopa | walimwogopa | walimwogopa |
| 5. | wao | kwa | yao | wetu |
| 6. | moja moja | mmoja | moja | mumoja |
| 7. | mshipa | msiba | mwiba | mshiba |
| 8. | mwingine | kivani | mwisho | kifani |
| 9. | alimwingia | ilimwingia | ulimwingia | lilimwingia |
| 10. | kwenye | ndani | hadi | mbaka |
| 11. | hii | huyu | huyo | huu |
| 12. | shimoni | pango | pangoni | tunduni |
| 13. | ilikuwa | ilikua | ilikua | lilikuwa |
| 14. | kusisitisha | kusisitiza | kusikitisha | kuzizitisha |
| 15. | unapostaajabu | unapoajabishwa | ukistaajabu | ukistajabu |

**Kuanzia swali la 16 - 30, changua lililo sahihi :-**

16. Sabalkheri Juma, Je Juma alikutana na rafikiye wakati upi?
 A. Alasiri B. adhuhuri
 C. alfajiri D. jioni

17. Bainisha matumizi ya neno lililopigwa mstari katika sentensi
 Mwalimu <u>hodari</u> hutuzwa zawadi nyingi
 A. kielezi B. kihusishi
 C. kiwakilishi D. kivumishi

18. Chagua wingi wa "mtume huyo ana tunda hili"
 A. Watume hao wan amatunda haya
 B. Mitume hao wana matunda haya
 C. Mitume hao wana matunda hizi
 D. watume hao wana matunda haya

19. Walijibu kwa "jumla", maana yake ni
 A. haraka B. wamoja
 C. peke yao D. pamoja

20. Msimu huu ni wa kiangazi, mimea ____________
 A. imeota B. imenyauka

C. imekauka D. imestawi

21. Kamilisha tashbihi ifuatayo. Hakika kama _______

A. mauti B. ibada

C. ng'onda D. fungo

23. Neno lipi kati ya haya halipo katika ngeli ya U- Zi

A. wavu B. ulimi

C. ugonjwa D. ukuta

24. Nywele ziotazo juu ya kidevu na chini mdomo huitwa

A. malaika B. kionja mchuzi

C. sharafa D. kidaka tonge

25. Ndugu Opiyo ni mlingoti kijijini mwao. Ni mbinu ipi iliyotumika hapo juu?

A. Istiara B. semi

C. methali D. tashihi

26. Fundi wa kuwatahiri vijana huitwa__________

A. kuungwi B. jando

C. hamali D. ngariba

27. Chagua kielezi katika sentensi hii

"Mtoto wa Bakari huja hapa mara kwa mara"

A. mara kwa mara B. hapa

C. mtoto D. bakari

28. Umbo mkate pia huitwa ____________.

A. Tao B. duara

C. hori D.mstatili

29. Kamilisha tamakali ifuatayo

Machozi yalimpukutika ____________

A. chiriri B. kupukupu

C. kwi kwi kwi D. pukupuka

30. Kanusha sentensi ifuatayo

Wewe utapeleka barua

A. Wewe usingeleke barua

B. Wewe hujapeleka barua

C. Wewe hautapeleka

D. Wewe hutapeleka barua

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali 31-40:-**

Ndugu zangu waadhama, leo nawauliza,
Huku limbu na Giriyama, wote mpate sikia,
Wazima hata vilema, rai zenu nanuia,
Kipi cha kumpa, iwe ni yake fidia?

Miezi tisa tamima, tumbo lake nakalia,
Kwa uwezo wa karima, maama akajizalia,
Ni mdogo sijasema, shida zangu ajulia
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Mate kwake ni metema, mama hakunichukia,
Tumbo langu likiuma, kinyesi, namtupia,
Chakula hukuninyima., na dawa ya malaria,
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

Ni mtu mwenye huruma, tena wa kuvumilia,
Hasa uwe ni yatima, baba amejifia,
Akufanyia huruma, mradi kutimizia,.
Kipi cha kumpa maam, iwe nini yake?

Japo nimpe heshima, sioni kama murua,
Wema wake nikipima, mbali bado huitia,
Kunipa nyingi hiduma, mnini nitamlipia
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

31. Shairi hili ni la bahari gani?

A. Takhmisa B. guni

C. tarbia D. tasdisa

32. Malenga ana lengo gani katika shairi hili?

A. hadhi anayestahili mama

B. adhabu ya mama

C. mtoto mtukutu na mama

D. kazi ya mtoto kwa mama

33. Sehemu ya kwanza ya mshororo wa ubeti huitwa_____

A. utao B. ukwapi

C. mwanzo D. mwandamizi

34. Shairi lenye vipande vitatu huitwaje?

A. utenzi B. ngonjera

C. ukawafi D. mathnawi

35. Ubeti wa pili una jumla ya mizani mingapi?

A. 16 B. 32

C. 63 D. 64

36. Ni lipi si jina la mshororo wa mwisho wa ubeti?

A. Ukwapi B. Mkarara

C. Kipokeo D. Kibwagizo

37. Shairi lenye mishororo mitano katika ubeti ni ______

A.Takhmisa B. Tarbia

C. Tasdisa D. Tathnia

38. Stadi wa kutung ana kuiba mashairi huitwawa______

A. Mtunzi B. sogora

C. Manju D. malengo

39. Shairi zima lina mishororo mingapi?

A. 16

B. 20

C. 4

D. 64.

40. Bila kokoma ni sawa na

A. Bila kuzeeka

B. Bila kukataa

C . Bila kuona

D. Bila mwisho

**Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 41- 50**

Ulimwengu unazidi kubadilika kila uchao. Mabadiliko haya hasa hutokana na teknolojia geni ambayo imezidi kuboresha na kuzirahimishia shughuli za binadamu.

Mwanzo kabisa kulivumbuliwa simu ya mikoni. Simu hizi ambazo huitwa rununu au simu tamba zimerahisisha hali ya mawasiliano kabisa. Kwa kutumia simu hizi unaweza kuwasiliana na walio mbali kabisa bila kutumia nyaya. Unaweza pia kuwasiliana na aliye mbali kwa kutumia ujumbe mfupi kwa gharama ndogo sana rununu pia, hutumiwa kama redio na kamera ya kupigia picha

Chombo kingine ni tawakilishi, chombo hili cha mawasiliano hutumia ofisi omi na hata nyumbani. Trarakilishi hupiga chapa hufanya hesabu na kuhifadhi maandishi . Maaandishi haya hulifadhiwa katika disketi tepetevu.

Chombo kingine cha mawasiliano ni wavuti. Kwa kutumia mtandao wavuitia, unaweza kuwasiliana na yeyote aliye popote duniani na wakati wowote kwa hivyo, sio watu wengi wanaoendelea kutumia masanduku ya posta.

Runing anayo ni chombo kinachotoa sauti pamoja na kuonyesha picha zenyewe. Runinga hupendwa sana kwa sababu mawasiliano yake ni ya moja kwa moja na matangazo yake huwafikia watu wengi wakati mmoja. Runinga pia hutumika kuonyesha vipindi vya kuelismisha na kuburudisha mno.

41. Vifuatavyo ni vyombo vinavyotokana na teknolojia ya kisasa isipokuwa

A. tarakilishi B. runinga

C. rununu D. redio

42. Zifuatazo ni kazi ya rununu ila

A. kutumia ujumbe mfupi

B. kupiga picha

C. Kupiga chapa

D. Kuwafiliana na aliye mbali

43. Ni chombo kipi kinachotumika kupiga chapa, kuhifadhi maandishi na kufanya hesabu?

A. tarakilishi

B. rununu

C. kamera

D. runinga

44. Kulingana na habari

A. sio watu wnegi wanaotumia mnasanduku ya posta

B. Mtao wavuti hupatikana kila mahali

C. Watu wengi hutumia masanduku y aposta

D. Mtandao wavuti ni ghali mno

45. Ukitaka kupasha ujumbe kwa watu wengi tena wakati mmoja, utatumia

A. rununu B. runinga

C. mtandao wavuti D. tarakilishi

46. Neno jingine lenye maana sawa na tarakilishi ni

A. komput a B. kamera

C. kompyuta D. chompyuta

47. Ni chombo kipi kinachotoa sauti na kuonyesha picha wakati mmoja?

A. runinga B. redio

C. Rununu D. sanduku la posta

48. Ukitaka kuona vipindi vya kuburudishha na kuelimisha anaweza kutumia

A. tarakilishi B. Runinga

C. Redio D. Kamera

49. Ni chombo kipi kilivumbuliwa kwanza?

A. Runinga B. Tarakilishi

C. Rununu D. wavuti

50. Kichwa kinachofa habari hii ni

A. Elimu ya kisasa

B. Mawasiliano

C. Ulimwengu wetu wa kisasa

D. Teknolojia ya kisasa